

# Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA MUHULA WA PILI – 2023

---

**102/1**                      **Kiswahili – Insha**                      **Karatasi ya 1**  
**KIDATO CHA TATU**                      **JULAI/AGOSTI, 2023**                      **Muda:Saa 1 ¾**

---

## KARATASI YA KWANZA 102/1MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

---

1. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Elimu kuchunguza njia za udanganyifu katika mitihani ya kitaifa. Andika kumbukumbu za mkutano wa kuwasilisha uchunguzi huo.

**Tanbihi:** Mwanafunzi asiandike insha ya Ripoti.

Hii ni insha ya kumbukumbu.Mtahiniwa azingatie vipengele muhimu.

1. Kichwa

- Jina la mkutano
- Mahali pa mkutano
- Siku ya mkutano
- Tarehe ya mkutano
- Saa

2. Utangulizi

- Waliohudhuria
- Waliotuma udhuru
- Waliokosa kuhudhuria
- Waalikwa

3. Mwili

I .Ajenda

- Kufunguliwa kwa mkutano
- kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za mkutano uliotangulia
- Yaliyotokana na kumbukumbu hizo
- (Ajenda zinazohusu njia mbalimbali wanafunzi wanatumia kuiba mtihani)
- masuala mengine
- kufungwa kwa mkutano

4. Hitimisho

Sehemu za katibu na mwenyekiti kuachwa wazi na tarehe.

Mwili/Maudhui

**a). Njia za udanganyifu**

- a. Matumizi ya rununu. Kuwasiliana na wengine wa mbali kuhusu maswali ya mtihani.
- b. Walimu kuwasaidia kufanya mtihani kisha wanawapatia majibu.
- c. Wanafunzi wa vidato vingine kuwafanyia mtihani.
- d. Kusaidiana kwa watahini wenyewe katika cha mtihani n.k
- e. Kusoma kutoka vitabuni na vijikaratasi walivyovitiyarisha mapema.
- f. Kutoa majibu mtandaoni.
- g. Kupiga maswali na majibu picha

**2. Serikali ndiyo ya kulaumiwa kutokana na kupanda kwa gharama ya maisha nchini Kenya**

**Jadili.**

Hii ni insha ya mjadala. Iwe na muunda ufuatao;

- i. **Kichwa**- Mtahiniwa abuni kichwa mwafaka kulingana na swali
- ii. **Utangulizi**- Mtahiniwa atangulize insha yake kwa kufafanua suala la kupanda kwa gharama ya maisha na mchango wa serikali katika kuishulikia.
- iii. **Mwili**- Maudhui yajitokeze hapa. Mtahiniwa aandike hoja za kuunga mkomo kauli hii na zile za kupinga.

**Kuunga mkono( serikali imechangia vipi)**

- a) Kuongeza bei ya bidhaa ya kimsingi k.m mafuta.
- b) kufutilia mbali ada za huduma za kimsingi kama vile matibabu, elimu, n.k
- c) Kuruhusu wengine kukwepa ulipaji wa ushuru.
- d) Kutopanua nafasi za kazi/ajira.
- e) Kulegea katika kupambana na tatizo la ufisadi.
- f) Kukosa kuhimiza wananchi na mashirika mbalimbali kubuni nafasi za kazi.
- g) Kuongeza wafanyikazi kupita kiasi katika idara mbali mbali za serikali kuu na kaunti.

**Kupinga ( sababu zingine kando na jukumu la serikali)**

- a) Mabadiliko ya tabia nchi. k.m hali ya anga
- b) Kuzorota kwa uchumi duniani
- c) Kuzembea kwa wananchi huku wakitegemea usaidizi na misaada.
- d) Majanga yasiyozuilika k.m Korona

**3. Tunga kisa kitakachodhihirisha matumizi ya methali ifuatayo:**

**Jifya moja haliinjiki chungu.**

Hii ni insha ya methali.

Mtadiniwa abuni kisa kitakachodhihirisha maana ifuatayo: Hamna mtu anayefanya mambo pekee akaweza kufaulu.

Hivyo anaweza kutunga kisa kinachosimulia:

*(a) Mtu aliyekataa kushirikiana na wengine kufanya mambo fulani na mwishowe akashindwa kufaulu.*

*(b) Ushirikiano katika jamii k.v. shule, kijijini, nyumbani n.k. ulioleta faida.*

#### 4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno yafuatayo:

**Kweli nimetambua kuwa, familia ni nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii.**

Mwanafunzi anahitajika kutunga kisa kinachoonyesha nafasi ya familia katika kujenga jamii.

Visa vifuatavyo vinaweza kudhihirika:

- i) Kisa cha familia kinachosomesha wana wao na kuwapa wosia ya kuishi vyema. Familia hiyo ikawa taa katika mazingira ambayo yalikuwa na matatizo awali.
- ii) Kisa cha familia inayopuuza majukumu yake. Hivyo, wanafamilia hiyo kuwa tatizo sugu kwa jamii pana.